# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA

## 1.0 Utangulizi

Andiko hili lina ainisha maeneo ya uwekezaji kiuchumi na huduma kwa wawekezaji wa ndani (wazawa) na wa nje (nje) yaliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya singida katika sekta mbalimbali.

Kupitia sekta hizi, halmashauri imedhamiria kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya watu kama ambavyo dhima ya Halmashauri ilivyojikita katika kuimarisha utawala bora na ushiriki wa wananchi katika ngazi zote za maamuzi na kuboresha maisha ya watu kwa kuleta maendeleo endelevu.

Maeneo ya kipaumbele ya kiuchumi yaliyoainishwa ni pamoja na Kilimo, uchimbaji madini (ya ujenzi), uvuvi, usafirishaji, utalii na viwanda wakati maeneo ya huduma ni sekta ya afya na Elimu.

### Eneo la Kiutawala

Halmashauri ya Manispaa ya Singida ni moja kati ya halmashauri 7 za Mkoa wa Singida yenye ongezeko kubwa la watu. Aidha ni moja ya Halmashauri 2 zilizopo katika wilaya ya singida yenye jimbo moja la uchaguzi, tarafa 2, Kata 18, Vijiji 19 vitongoji 53 na mitaa 87. Halmashauri ya Manispaa ya Singida ni miongoni mwa Wilaya zenye fursa za uwekezaji na imeendelea kukua vizuri kiuchumi kupitia uwekezaji katika Sekta ya Viwanda. Manispaa ina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 754 na limezungukwa pande zote na eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Kati ya eneo la kilomita za mraba 754:

| | |
|---|---|
| • Eneo linalofaa kwa kilimo $Km^2$ | 293.5 |
| • Eneo linalofaa kwa malisho $Km^2$ | 246.1 |
| • Eneo la maji $Km^2$ | 23.5 |
| • Eneo la misitu na vichaka $Km^2$ | 58.7 |
| • Mengineyo $Km^2$ | 35.2 |
| • Makazi $Km^2$ | 97.0 |
| **Jumla** | **754** |

**Idadi ya watu:**

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Manispaa ya Singida ilikuwa na wakazi 187,563 wakiwemo wanawake 95,748 na wanaume 91,845. Ongezeko la watu ni wastani wa asilimia 2.71.

Hata hivyo kwa makadirio ya hivi karibuni (2022) Idadi ya watu inakadiriwa kufikia 192,975 .

## 2.0 Sekta kuu za kiuchumi

Kulingana na eneo la kijiografia la halmashauri ya manispaa ya singida, shughuli kuu za kiuchumi ni pamoja na Kilimo, ufugaji, uvuvi, usafirishaji, biashara ndogondogo na za kati shughuli za uchimbaji madini ya ujenzi na uendeshaji viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Hata hivyo shughuli kuu katika Halmashauri hii ni biashara ambayo huchangia katika pato la ndani la manispaa.

### 2.1 Kilimo

Uzalishaji wa mazao ya kilimo

Shughuli kuu katika sekta hii ni uzalishaji wa mazao ya kilimo na biashara eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta hekta 29,400 ambapo eneo linalotumika kwa kilimo ni hekta 12,500 sawa na asilima 43 ya eneo lote. Mazao ya chakula yanayolimwa ni pamoja na mahindi, mihogo, maharage, mtama, uwele, viazi vitamu, na mbogamboga. Kwa upande wa mazao ya biashara yanayolimwa ni ulezi, Alizeti, na mbogamboga.

**Ufugaji**

Ufugaji ni shughuli mojawapo inayochangia kwa kiasi kikubwa katika mapato ya ndani katika halamshauri ya manispaa ya singida. Eneo la malisho kwa ajili ya mifugo ni 246.1 km2 sawa na 34% ya ukubwa wa eneo la Manispaa. Halmashauri ina jumla ya ng'ombe 47,620 Mifugo mingine ni mbuzi 36,444, kondooo 13,966 nguruwe 906, mbwa 2,951 na kuku 53,893 wa kienyeji na wa kisasa. Aidha Manispaa ya Singida imekuwa kitovu cha soko la mifugo kutokana na Manispaa hii kuwa makao makuu ya mkoa wa Singida na minada ya mifugo kuhusisha Wafanyabiashara kutoka Sehemu mbalimbali.

## 2.2 Misitu

Misitu ya kiasili ni eneo muhimu sana la kiuchumi. Halmashauri ya Manispaa ya Singida inayo maeneo 58.7 ya misitu ya asili ambayo ni Mwankoko, Mtamaa, Uhamaka, Mtipa, Unyianga, Unyamikumbi, Unyambwa na Kisaki. Mazao yanayotokana na misitu ni pamoja na nguzo, kuni, asali na nta. Wastani wa uzalishaji wa Asali kwa mwaka ni tani 14 na nta ni kilo 900. Uzalishaji wa nguzo (milunda) upo katika Kata za Mungumaji, Unyambwa na Unyamikumbi ambapo kuna mashamba ya miti ya mikaratusi inayozalisha nguzo.

## 2.3 Uvuvi

Sekta hii ni miongoni mwa sekta za kiuchumi zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika kutoa ajira. Eneo la halmashauri ya manispaa lipatalo kilometa za mraba 23.5 zimefunikwa na maji. Aidha Manispaa ya Singida inayo maziwa 02 ya Kindai na Singidani yanatumika kwa shughuli za uvuvi na burudani. Jumla ya mialo 2 inapatikana katika maziwa haya yanayotoa samaki aina ya perege (tilapia) wanaokidhi soko la ndani ya manispaa. Hata hivyo ipo fursa katika maziwa hayo ya ufugaji wa samaki kwa njia vizimba (cage fishing). Jumla ya tani zipatazo 35 za samaki huvuliwa kila mwaka kupitia uvuvi wa asili.

## 2.4 Utalii

Sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta ya kiuchumi katika halmashauri ya manispaa ya singida ambayo imejaliwa kuwa na vivutio mbalimbali kama Ndege, Maua, misitu ya asili, tamaduni za makabila ya kinyaturu na kinyiramba, urithi wa historia za kuvutia za watawala wa kimila wa

kabila la kinyaturu, mawe makubwa, michoro ya kale na mahandaki ya kihistoria.

## 2.5 Uchimbaji wa madini ya ujenzi

Halmashauri ya Manispaa ya Singida inajivunia uwepo wa madini ya ujenzi katika maeneo mbalimbali ya manispaa hii. Maeneo yanayojishughulisha na uchimbaji wa madini ya ujenzi ni pamoja na Kata ya Mungumaji, Kisaki, na Unyianga. Uwepo wa shughuli za uchimbaji wa madini ya mchanga na kokoto umetoa fursa ya ajira, biashara nk kwa wakazi wa maeneo mbalimbali ya Manispaa ya singida.

Uwekezaji katika sekta ya madini ni uchakataji wa kokoto (Coarring)

## 3.0 Miundombinu

Halmashauri ya Manispaa ya singida inahudumiwa na mtandao wa barabara unaokisiwa kufikia jumla ya km. 523 kati ya hizo km. 20 ni barabara za lami, barabara za changarawe km. 86. Asilimia 20 ya barabara za vijijini zinapitika katika majira yote ya mwaka.

Kwa upande wa nishati ya umeme, Manispaa ya Singida kupitia mradi wa umeme vijijini REA imefanikiwa kufikisha umeme katika Vijiji 15 kati ya 19 na mitaa 44 kati ya 53 zoezi la usambazaji umeme linaendelea katika maeneo ambayo hayafikiwa.

Aidha upande wa mawasiliano ya simu na posta Halmashauri ya Manispaa ya Singida ni miongoni mwa halmshauri za manispaa ya singida zinazofaidika na huduma hizo kwa mapana zaidi. Kampuni zinazotoa huduma hizo ni pamoja na TIGO, VODACOM, AIRTEL, HALOTEL na TTCL. Aidha huduma za kibenki zinapatikana kutoka Bank ya NMB, NBC, CRDB, Bank ya POSTA na DTB.

## 4.0 maeneo mahsusi ya uwekezaji

Maeneo mahsusi ya kiuchumi ya uwekezaji yaliyoainishwa ni pamoja na Kilimo cha zao la kimkakati la Alizeti, Ufugaji, Uvuvi, Misitu na Ufugaji nyuki, kilimo cha mbogamboga, viwanda na uchakataji madini ya ujenzi. Kwa upande wa uwekezaji wa maeneo ya huduma ni katika sekta za elimu na afya.

### 4.1 kilimo cha kimkakati cha alizeti

Kilimo cha alizeti ni fursa muhimu ya uwekezaji katika Manispaa ya singida.

- Aina ya uwekezaji inayotarajiwa hapa ni uwekezaji katika kilimo na viwanda kwa ajili ya kusindika mafuta ya alizeti na chakula cha mifugo (mashudu).
- Wawekezaji wanaopendekezwa katika eneo hili ni wakulima wakubwa wenye mtaji mkubwa watakaoweza kuwatia hamasa wakulima ili kuweza kuboresha uzalishaji pia uwekezaji wa viwanda Vidogo, vya kati na vikubwa.
- Maeneo yanayofaa kwa uwekezaji wa aina hii ni **Kata ya Mwankoko, Mtamaa, Unyianga, Uhamaka, Unyamikumbi, Mtipa, Mungumaji, Kisaki na Unyambwa** yanayofanya jumla ya **hekta 29,400**. Aidha tani za alizeti zinazotarajiwa kuzalishwa ni **88,200** ambazo zinatarajiwa kuzalisha mafuta lita **26,460,000** Kwa mwaka.






### 4.2 kitenga uchumi cha biashara

Manispaa ya Singida inalo eneo katikati ya mji kwa ajili ya kitega uchumi. Eneo hili ni mahususi kwa ajili ya Biashara (Prime area)

**Aina ya uwekezaji**: Uwekezaji unaotarajiwa ni ujenzi wa jengo la kitegauchumi kwa ajili ya maduka, kumbi za mikutano na sherehe na ofisi mbalimbali.

**Wawekezaji wanaopendekezwa:** Wawekezaji wanaotarajiwa ni wakubwa na wa kati wenye mitaji kwa ajili ya ujenzi wa kitegauchumi.
**Eneo husika**: Eneo la Stendi ya zamani lenye ukubwa wa mita za mraba 10,989 katika kata ya Majengo

### 4.3 ufugaji na uchakataji wa mazao yatokanayo na mifugo

Ufugaji ni shughuli yenye umuhimu katika Halamshauri ya Manispaa ya Singida.
**Aina ya uwekezaji**: Ufugaji na uwepo wa viwanda vya kuchakata na kufungasha mazao yatokanayo na mifugo kama ngozi, nyama, maziwa na mbolea pia wawekezaji wa kuzalisha vifungashio vya mazao ya yatokanayo na mifugo.
**Wawekezaji wanaopendekezwa**: wawekezaji wakubwa, kati na wadogo
**Maeneo yanayofaa**: Kata ya Kisaki eneo la Ng'aida ambalo tayari limepimwa na lina hati . Ukubwa wa eneo ni ekari 7.



### 4.4 uvuvi

Uwepo wa Maziwa Kindai na Singidani ni fursa nyingine kubwa iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida
**Aina ya wekezaji**: katika sekta hii ya kiuchumi uwekezaji wa ufugaji Samaki katika vizimba (cage fishing), uvuvi kwa kutumia teknolojia ya kisasa, usindikaji wa samaki pia ufugaji wa Samaki kwa njia ya mabwawa ya kuchimba.

**Wawekezaji wanaotarajiwa**: ni wale wa Kati na wadogo ambao wataweza kuwekeza katika uvuvi, usindikaji mazao ya Samaki na usambazaji wa nyenzo za uvuvi.
**Maeneo yanayofaa**: Maeneo yanayopendekezwa kwa uwekezaji huu ni Kata ya Kindai na Mughanga ambapo yanapatikana maziwa ya Singidani na Kindai. Jumla ya tani 35 za samaki zinatarajiwa kuzalishwa kwa mwaka.



**4.5 uzalishaji na uchakataji wa mazao ya nyuki**
Uwekezaji katika uzalishaji wa mazao ya nyuki ni fursa ya kiuchumi katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida. Manispaa ya Singida ina misitu ya asili aina ya miombo katika Kata za Mwankoko, Uhamaka, Mtamaa, Mtipa, Kisaki na Unyianga. Misitu hii inaweza kutumika kwa uzalishaji wa mazao ya nyuki ambayo ni asali na nta. Uchakataji wa mazao ya nyuki ni fursa nyingine ya uwekezaji katika sekta ya Ufugaji nyuki ambapo wafugaji wengi wa nyuki huuza mazao yao yakiwa hayajachakatwa na kufungashwa vizuri.
**Aina ya uwekezaji**: Uhitaji wa viwanda vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki (Asali na Nta) ni mojawapo ya fursa ya uwekezaji.
**Wawekezaji wanaopendekezwa**: wawekezaji wakubwa watakao wekeza katika viwanda kwani kwa sasa kuna kiwanda kimoja tu cha kuchakata mazao ya nyuki.

**Maeneo yanayofaa**: Kata za Mwankoko, Uhamaka, Mtamaa, Mtipa, Kisaki na Unyianga



### 4.6 utalii wa asili na hoteli za kitalii

Fursa hii itatoa mwanya kwa wawekezaji wakubwa na wa kati kuwekeza katika shughuli za kitalii ikizingatiwa kuna maeneo mazuri ya kiasili ambayo hayajaguswa yenye kuvutia na yenye historia ya kipekee.

**Aina ya uwekezaji**: ni ujenzi wa hoteli za kitalii, uanzishwaji wa kambi za kitalii (camp sites), huduma za watalii (tour guide and travel services), upandikizaji wa Wanyama waishio majini na Ndege pia michezo ya makasia (canoeing) pamoja na uboreshaji wa mandhari ya fukwe.

**Maeneo yanayopendekezwa**: kwa uwekezaji wa hoteli za kitalii ni Kata za Mughanga, Mitunduruni, Kindai, utemini, Ipembe na unyambwa



## 4.7 Nishati

Uwekezaji katika nishati ya umeme ni muhimu ili kuwezesha uendeshaji wa shughuli za uzalishaji na utoaji wa huduma.

**Aina ya uwekezaji:** Uwekezaji unaotarajiwa hapa ni uwekezaji katika nishati ya umeme wa jua na upepo.

**Wawekezaji wanaopendekezwa:** wakekezaji wakubwa na wa kati wenye uwezo wa kusambaza nishati hii**.**

**Maeneo yanayopendekezwa**:

(i) Uwekezaji wa umeme wa upepo; Kititimo hekta 600, Unyamikumbi hekta 1621, Kisaki 501, Kisasida hekta 665.

(ii) Uwekezaji wa umeme wa jua;Unyambwa hekta 38.6, Manga hekta 1075, Unyinga hekta 250.

## 5.0 Uwekezaji katika maeneo ya huduma

Pamoja na uwekezaji katika maeneo ya kiuchumi, Halmashauri ya Manispaa ya Singida inaalika/kukaribisha wawekezaji pia katika sekta / maeneo ya huduma kama vile Afya na Elimu

## 5.1 Sekta ya afya

Uwepo wa huduma za afya za kutosheleza ni muhimu sana kwa ukuaji na maendeleo ya jamii katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida. Ili jamii iweze kushiriki kikamilifu katika uzalishaji ni lazima wawe na afya. Manispaa ya Singida ina jumla ya vituo vya huduma za afya kati ya hivyo vituo vya afya ni 1 na zahanati 9 zahanati za serikali…. za binafsi….).

**Aina ya Uwekezaji:** Uwekezaji unaotarajiwa ni ule wenye kutoa huduma za uhakika na za kutosheleza.

**Wawekezaji wanaopendekezwa:** wawekezaji wanaotarajiwa ni wale wakubwa na wakati ili kuwekeza katika huduma za vituo vya afya, zahanati, maabara za kisasa, duka la dawa la wilaya litakalaosambaza dawa katika vituo vyote vya huduma. Aidha, Halmashauri pia inaalika wawekezaji watakaowekeza katika kuongeza nguvu (support) katika miradi ya serikali na wananchi kwa kuendeleza jitihada za ujenzi zilizokwisha anzishwa.

**Maeneo yanayopendekezwa:** kwa uwekezaji huu ni katika kata zote zisizokuwa na zahanati na vituo vya afya.




## 5.2 Sekta ya elimu

Halmashauri ya Manispaa ya Singida ni moja kati ya Halmashauri 7 za mkoa wa Singida yenye ongezeko kubwa la idadi ya watu ukilinganisha na halmashauri zingine katika mkoa wa Singida. Ongezeko hili ni kutokana na jamii kuzaliana kwa kasi, kuwepo kwa wageni wengi

wanaoingia na kutoka pamoja na shughuli mbalimbali za kiuchumi ikizingatiwa Manispaa ni kitovu cha mkoa wa singida ambapo njia kuu kuelekea mikoa ya kanda ya ziwa, mikoa ya kaskazini mwa nchi na mikoa ya kanda ya magharibi na pwani hupita Manispaa ya Singida.

Kutokana na hali hii sekta ya elimu imeonekana kuelemewa katika kutoa huduma kutokana na upungufu wa miundombinu. Kwa upande wa elimu ya msingi, Halmashauri ya Manispaa ina jumla ya shule **71** za msingi zenye jumla ya wanafunzi **47,404** wavulana wakiwa **23,515** na wasichana **23,889** kati ya hizo shule 53 ni za serikali na **18** ni za binafsi
Halmashuri ya Manispaa inaalika wawekezaji wakubwa na wakati kuwekeza katika eneo hili la huduma. Pia kuwekeza katika katika ujenzi wa Miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ambayo ni vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na madawati miradi iliyokwisha anzishwa na Serikali ama wananchi.



Kwa upande wa shule za sekondari Halmashauri ya Manispaa ina jumla ya shule za sekondari **18** ambazo pia zinahitaji kuongezewa nguvu (support) ili huduma hii ya elimu ya sekondari iweze kuimarika. Nguvu (support) inayohitajika katika eneo hili ni ukamilishaji wa vyumba **27** vya

maabara, ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa **64**, nyumba za walimu **321**, uanzishaji wa shule zenye kidato cha 5&6 (High School), vyoo matundu **565**, viti **12,515** na meza **12,515** kwa ajili ya wanafunzi ikiwa ni kuunga mkono jitihada za wananchi na Serikali katika kutoa elimu bora na sio bora elimu.



Aidha Halmashauri ya Manispaa ya Singida inakaribisha wawekezaji katika kuwekeza katika vyuo vya ufundi (technical/ vocational centres). Eneo hili ni muhimu kwani Halmashauri ya Manispaa ina uhaba wa vyuo vya ufundi. Kutokana na fursa zilizopo ujuzi unahitajika ili kuongeza ajira kwa Vijana. Fursa hizo ni kama elimu ya kuchakata madini ya ujenzi ( kokoto), kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi na mifugo, usindikaji wa mafuta ya alizeti, samani za nyumbani na ofisi na shule, mazao yatokanayo na nyuki n.k

Aina ya wawekezaji: Wawekezaji wanaohitajika / kupendekezwa ni wale wakubwa na wa kati wenye uwezo wa kuwekeza katika kuanzisha vyuo

vya ufundi, elimu ya juu ya sekondari, na kuunga mkono jitihada za jamii na serikali kwa kuendeleza / kukamilisha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia iliyokwisha anzishwa.

Maeneo yanayopendekezwa/ kutengwa: kwa uwekezaji huu ni Mwankoko **hekta 250**, Manga **hekta 400**, Mtamaa **hekta 550**

